

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE**

**07 MEI, 2026**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA TATU

**KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE – TAREHE 07 MEI, 2026**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

#### **IV. MASWALI YA KAWAIDA:**

##### **OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):**

##### **267. MHESHIMIWA ARIF SULEIMAN PREMJI (MTWARA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Shule ngapi za Kidato cha Tano na Sita zimejengwa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 hadi kufikia robo ya pili - Mtwara Vijijini.

##### **268. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, kwa nini Serikali isiondoe Mfumo wa Wanafunzi kurudi mchana kula nyumbani na kurudi tena Shuleni ili kuongeza kiwango cha ufaulu kwa Wanafunzi.

##### **269. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatimiza ahadi ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mtitaa - Bahi.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**270. MHESHIMIWA ONESMO MERDSON MNKONDYA (MBOZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itajenga Chuo Kikuu katika Mkoa wa Songwe.

**WIZARA YA UJENZI:**

**271. MHESHIMIWA MORRIS JOSEPH MAKOI (MOSHI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itamrejsha Mkandarasi wa Barabara ya Moshi *International School* - Kibosho kwa Rafael yenye urefu wa Km 5.49

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**272. MHESHIMIWA MWINYI JAMAL RAMADHAN (BUMBWINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni Wanyama gani wana vibali vya kuwindwa kwa matumizi ya Kijamii kwa kuwa nchi yetu ina Wanyama wengi katika mapori ya Vijijini.

**273. MHESHIMIWA KANGI ALPHAXARD LUGOLA (MWIBARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti kero ya Mamba wanaodhuru Wananchi.

**WIZARA YA MADINI:**

**274. MHESHIMIWA MWANAHAMISI ATHUMANI MUNKUNDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, upi mpango wa kuanzisha Kituo cha Umahiri eneo la Mwakitolyo kutokana na ushiriki mkubwa wa Wanawake na Vijana katika uchimbaji wa madini.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**275. MHESHIMIWA HAPPINESS DANIEL NGWANDO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha Sheria ya Ndoa pale wanandoa wanapotalikiana ili kumaliza kesi zao haraka.

**276. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY  
(MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mbulu ambao umesimama kwa muda mrefu.

**V. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**DODOMA  
07 MEI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD  
KATIBU WA BUNGE**